

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA**

**MAAGIZO KWA WANACHUO WA MWAKA WA PILI MUHULA WAKWANZA
TAREHE 31/07/2020**

Ada ya Chuo ni **450,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza ulipwa kwa awamu mbili yaani **225,000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote **450,000/=** kwa mwaka. Ada ilipwe baada ya kupata namba ya kumbukumbu (Control number) toka kwa mhasibu wa chuo ndugu **Makuru Mohamedi Temambele (0786 441 736)**.

Michango ya Chuo kwa wanachuo wote ilipwe kwenye akaunti ya michango **NMB AKAUNTI Na. 31101200023** yenye Jina **Butimba Teachers Training College**. Michango hiyo ni kama ifuatavyo:

NA.	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo (SEWABU)	5,000	Kwa mwaka
2	Huduma ya kwanza	10,000	Kwa mwaka
3	Usafi na mazingira	20,000	Kwa mwaka
4	Kukodisha godoro	10,000	Kwa mwaka
5	Michezo	30,000	Kwa mwaka
6	Ulinzi	30,000	Kwa mwaka
7	Ukarabati	25,000	Kwa mwaka
	JUMLA	130,000.00	

Aidha, ada ya Mtihani wa Taifa (NECTA) wa **kidato cha sita** kwa wanachuo wa mwaka wa pili miaka mitatu, shilingi **50,000.00** ilipwe kwenye akaunti tajwa hapo juu kabla ya tarehe **30/08/2020**.

MUHIMU SANA:

Mwanachuo aje na **'Bank Pay in Slip'** au Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na **Stakabadhi/Pay in Slip** mbili, moja inayoonesha malipo ya ada na nyingine ioneshe malipo ya michango. Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zioneshe jina kamili la mwanachuo husika.

Inashauriwa uwe na kadi ya bima ya Afya kwa ajili ya uhakika wa huduma ya matibabu kutoka katika hospitali yoyote na mahali popote utakapokuwa. Ujapo chuoni uje na Bunda (01) la karatasi (DOUBLE A, NOPA, SMART COPY) na iwapo unadaiwa ada, michango au kifaa chochote kwa mwaka wa kwanza hakikisha unakamilisha.

TANBIHI: Wanachuo wote ambo hawajawasilisha vyeti halisi vya kuhitimu kidato cha Nne (Diploma Miaka 3), kidato cha Nne na Sita (Diploma Miaka 2) hata kama hakikutumika kuomba kujiunga na mafunzo ya ualimu, mnatakiwa kuwasilisha vyeti hivyo chuoni kabla ya tarehe **30/08/2020**.



Nicholaus A Magige

MKUU WA CHUO

**MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
S. L. P. 1411 MWANZA**